



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Henry J. Mroz Central Administration Offices
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Mei 29, 2020

Wapenzi Wanajamii wa Shule za Lowell Public Schools,

Tunatarajia kwamba nyinyi na wapenzi wenu mko salama na wenyе afya. Huku tukikamilisha Likizo la Memorial Day na tukikaribia mwanzo wa mwezi wa Juni, tuko karibu kumaliza mwaka wa shule. Bila shaka, hili lilikuwa mwaka wa shule tofauti kule mwaka mwingine wowote. Ni takriban miezi mitatu tangu shule kufungwa kote Massachusetts na bado tunaendelea kuhisi athari za COVID-19. Na ilihali gavana ametangaza kufunguliwa tena wa kiawamu kwa jimbo, kurudia kwa "hali ya kawaida" kwa sasa inaonekana itachukuwa miezi kadhaa yajayo.

Kutoka msimamo wa shule, ingawa hatukuweza kuwa katika majengo yetu tangu Machi, walimu wetu, walimu wakuu, makocha, wafanyakazi wa jamii, wafanyakazi wategemezi, wafanyakazi wa mkahawa, na washirika wa kijamii wameungana kutoa huduma muhimu na kubuni mbinu mpya za kuelimisha wanafunzi wetu. Najivunia sana na jamii nzima ya shule ambayo imefanya kazi bila kusita katika hali zisizo za kawaida.

Kama kikumbusho, siku ya mwisho ya mwaka wa shule wa 2019-2020 ni Jumatatu, Juni 15. Ni muhimu kwamba kati ya sasa na tarehe hiyo tuendelee na mwendo huo tulioanzisha na masomo ya mbali na tumalize mwaka wa shule na mwendo huo huo. Shule ya mtoto wako itawasiliana na wewe kuhusu lini inapoweza kurejesha mashine zozote ambazo uliazimwa na Lowell Public Schools na kuhusu lini mtoto wako anaweza kuchukuwa vitu zake alizoa cha kwa shule.

Katika majira ya kiangazi, tuko tayari kutoa programu zetu zote za kiangazi. Zikiwemo Kambi la IDEA au IDEA Camp ambacho hupendelewa – hii ni fursa yenye mwingiliano kwa wanafunzi wa shule ya kati na ya upili ili kuchunguza mada tofauti katika STEAM (Sayansi, Teknologia, Uhandisi, Sanaa na Hesabu). Sasa hivi tunapanga kufanya programu zote za kiangazi kutoka mbali. Lakini, kuna uwezekano wa mabadiliko ya kufanya katika mazingira ya shule kwa watu wachache katika kiangazi ambayo inahitaji mwongozo kutoka jimbo. Kujisajili katika Kambi la IDEA au IDEA Camp unaanza Juni 1, na taarifa zaidi inaweza kupatikana hapa: <https://www.lowell.k12.ma.us/ideacamp>. Programu zetu zinginezo za kiangazi zinaweza kupatikana katika tovuti ya wilaya: <https://www.lowell.k12.ma.us/summerprograms>

Kama ilivyo mila ya kila mwaka, huduma ya chakula itaendelea kiangazi na tutakujulisha pindi mahali na wakati wa huduma imepangwa.

Najua kila mtu anajuliza namna mwaka ujao utakua, na kama tutaweza kurudi katika majengo ya shule yetu. Hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya mwingiliano wa kila siku wa moja kwa moja unaotendeka kati ya walimu na wanafunzi katika mazingira ya shule ya kawaida, na

tungependa sana wanafunzi warudi madarasani mwao pamoja na walimu wao katika siku ya kwanza ya Septemba. Lakini, namna tunavyoendelea kuona, tunaweza kufanya hivyo pekee iwapo hali zinazozingira janga la COVID-19 zikiendelea kuboreka na hatari kwa jamii yetu ikipungua.

Tunapoongoja mwongozo wa ziada kutoka ofisi ya Gavana na kutoka maafisa wa afya wa jimbo kuhusu majira ya fall, tunashughulika katika mpango unaozingatia chaguo kadhaa za ufunguzi wa shule wa mwezi wa Septembaer ili tuwe tayari kikamilifu kuwashukuru wanafunzi wetu mazingira bora zaidi ya masomo inayowezekana katika hali ye yote ya usalama wa afya wa umma. Kwanza, kulingana na kitakachotendeka majira ya kiangazi – kuna uwezekano wa ufunguzi wa kikamilifu wa shule ikiwa na nyongeza za usalama. Uwezekano wa pili ambao hatupendelei tunayoweza kujipata katika ni – kulingana na data ya kiafya itakayotoka kati ya sasa na Septemba – ni haja ya kutendekeza chaguo la mafunzo ya mbali kikamilifu, itakayoboresha na kupanua yaliyokuwa yakifanyika miezi kadhaa zilizopita. Na uwezekano wa tatu ni mbinu ya kufanya mafunzo ya mbali pamoja na mafunzo katika shule, itakayotuwezesha kulinda umbali wa kijamii huku tukifanya masomo na wanafunzi wachache zaidi na jadwali ilio na nafasi. Tukiwa na mambo mengi hivi tusiyojuwa, kupangia killa uwezekano ni njia bora zaidi ili shule zetu ziwe tayari kikamilifu kuanza mwaka wa shule bila kujalisha hali ya janga ya COVID-19.

Kama wilaya, tumejifunza mengi sana tangu mwanzo wa kufungwa wa shule usiyoweza kueleweka, na hakuna kati yetu angeweza kukadiri mahali tulipo sasa. Kwa kweli hii imekuwa mwisho wenye changamoto kwa mwaka wa shule, lakini nataka kuwashukuru familia zetu zote, walimu, walimu wakuu, na wafanyakazi ambao wamechangia kuhakikisha uwezo wetu wa kutoa huduma muhimu kwa wanafunzi wetu na kuhakikisha watoto wetu wote wamepata fursa muhimu za masomo kutoka nyumbani. Nashukuru pia wote mliowasiliiana ili kuchangia fikra, kutoa maoni na kuuliza maswali. Ushiriki wenu umekuwa muhimu sana tukipitia kwa pamoja katika hali hizi zisizo za kawaida.

Ninaelewa kutokuwa na hakika kuhusu mwaka wa shule ujao unaoweza kuchangia katika wasiwasni na hali ya mkazo ambayo familia wanahisi kwa sababu ya janga hili. Tafadhali kumbuka kwamba tutaendelea kujulisha kila mtu tukitumia maelezo zaidi iwezekanavyo pindi tukizipokea. Wakati huu, unafaa kuwa na imani kamili ukijua kwamba shule za Lowell Public Schools zinapangia uwezekano wowote na tutakuwa tayari kuwashukuru watoto wetu uzoefu bora wa masomo utakayoweza kutarajia na wanastahiki huku pia tukihakikisha kwamba jamii yetu yote ikiendelea kuwa yenyeye usalama na afya sasa na majaliwa. Tutaendelea kuendelea mbele pamoja na kutegemezana kama wilaya moja, jamii moja na Lowell moja.

Wako Mwaminifu,



Dr. Joel D. Boyd
Msimamizi wa Shule